BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 08 Juni, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2023/2024.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

149. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Ujerumani ni miongoni mwa nchi ambayo ina uhaba wa mboga mboga na matunda. Na kwa kuwa nchi yetu ina fursa hiyo ya kilimo cha mboga mboga na matunda, bila ya shaka yoyote Balozi zetu zinazowakilisha Tanzania nchini Ujerumani, zina wajibu mkubwa wa kuhamasisha soko la kilimo hicho.

Je, Wizara yako inaitumia vipi fursa hii katika kuwaunganisha wazalishaji wa mboga mboga na matunda, ili wanufaike na fursa kama hizo kupitia balozi za Ujerumani na nchi mbali mbali duniani kote.

## Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

206. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Pamoja na kuzungumzia umuhimu mkubwa wa uhifadhi wa mazingira na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali bado haijalipa suala hili kipaumbele kinachostahiki na imekuwa ikitegemea zaidi misaada kutoka nje. Serikali yenyewe inatenga fedha kidogo sana kulingana na ukubwa wa jambo hili na athari zake mbeleni.

(a) Je, Serikali imetumia kiasi gani kwa kipindi cha 2020-2023 katika kutoa elimu kwa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

(b) Je, Serikali imetoa muongozo gani kuhakikisha kwamba shughuli za uwekezaji, utalii, kilimo, uvunwaji wa rasilimali za bahari na misitu na miradi ya maendeleo zinazingatia uhifadhi ya mazingira.

(c) Kwa kuwa Sheria Na.3 ya mwaka 2015 iliyoanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira imeanza kupitwa na wakati, Je, Serikali haioni haja ya kuipitia na kuifanyia marekebisho Sheria hiyo, ili iendane na wakati katika kusimamia shughuli za mazingira.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

217. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ili kuleta ufanisi na kuwafikia wananchi kwa karibu, Serikali hupeleka maafisa mbali mbali wa kisekta kwenye Ofisi za Wilaya. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kubwa ya rasilimali, nyenzo na uwezeshwaji wa maafisa hawa wa kisekta wanaopelekwa Wilayani.

(a) Je, Maafisa wa Kisekta (mfano maafa, uratibu wa shughuli za Serikali, mazingira, kilimo, ushirika, uwezeshaji, elimu, vijana, uvuvi na sekta nyengine) wanaopelekwa Wilayani wananufaika vipi na bajeti za Wizara zao za kisekta.

(b) Je, maafisa wa kisekta wanaopelekwa Wilayani wananufaika vipi na bajeti za Wilaya wanazozifanyia kazi.

(c) Kwa vile kuna kila ushahidi kwamba maafisa hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu na ya kudhalilika pamoja na kudharaulika bila ya kufikia malengo ya Serikali kiufanisi kama ilivyokusudiwa kwa kukosa rasilimali, nyenzo na uwezeshwaji. Je, ni upi utaratibu wa sasa wa kuziwezesha shughuli za maafisa hawa wakiwa Wilayani.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

125. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mwenendo wa biashara ya bima Zanzibar kupitia Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) unatia mashaka juu ya ubora na kukubalika kwa sera na mfumo wa kitaasisi na kisheria wa usimamizi wa biashara ya bima na hasa katika kuingiza faida kwa Serikali na wateja wenye imani tafauti.

(a) Je, ni ipi tathmini ya Serikali na wadau kuhusiana na mwenendo wa Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC).

(b) Je, Serikali haioni ulazima wa kupitia na kurekebisha sera na mfumo wa kitaasisi na kisheria wa udhibiti wa biashara ya bima Zanzibar.

(c) Je, ni upi mlinganisho wa kimaslahi wa wanachama wa Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) na makampuni mengine yanayoendesha biashara ya bima Tanzania.

<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>

193. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali imefanya juhudi kubwa ya kuwasogezea huduma mbali mbali yaani umeme, maji na kadhalika kwenye visiwa vyetu kama vile Tumbatu, Kojani, Uvinje na kwengineko. Hata hivyo, kuna changamoto ya kuendeleza huduma na miundominu yake kwa kukosekana mafundi walio karibu.

(a) Katika kuziendeleza na kuzidumisha huduma hizo, ni kwa nini Wizara haiajiri mafundi maalum katika visiwa hivyo, ili kuweza kukabiliana na changamoto mbali mbali za umeme na maji kwenye visiwa hivyo.

(b) Je, Serikali haioni kwamba kufanya hivyo kunaweza kuepusha majanga na maafa mbali mbali yanayosababishwa na nishati ya umeme na ukosefu wa maji ndani ya visiwa hivyo.

(c) Kwa kuwa katika kisiwa cha Tumbatu iko kamati maalum ya maji ambayo inapambana na changamoto hizo kwa sasa, Je, Serikali inaiangalia vipi kamati hiyo kwa kuipatia angalau sabuni ili kuongeza juhudi zaidi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

116. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa miezi ya hivi karibuni, kumekuwa na changamoto kubwa ya usafiri kati ya Pemba na Tanga, hali inayowapelekea wananchi wengi kutegemea usafiri wa majahazi ambao sio wa uhakika wala salama kwa maisha na mali zao.

(a) Je, ni sababu ipi iliyopelekea kukosekana kwa usafiri wa uhakika kati ya Pemba na Tanga kwa miezi ya hivi karibuni.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kuhakikisha kuwepo kwa usafiri wa uhakika na wa salama kati ya Pemba na Tanga.

(c) Je, kwa nini Serikali haiiruhusu ‘Mv. Sea Star’ kurudi kama zamani katika kutoa huduma za usafiri kwa Pemba na Tanga ili wananchi waweze kuepukana na usafiri wa majahazi.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

29. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Wali ndio chakula maarufu na muhimu kwa jioni ya Wazanzibari, ingawa bei ya mchele inapanda siku hadi siku na kuwafanya baadhi ya Wazanzibari washindwe kumudu mahitaji ya chakula hicho wanachokipenda angalau mara moja kwa siku.

Je, ni sababu gani ya msingi inayosababisha bei ya mchele wa mapembe kupanda siku hadi siku.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

195. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika ulimwengu wa sasa, kuajirika kwa wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vya kati kunategemea kwa kiasi kikubwa ujuzi ambao muhitimu anao na unaolingana na kazi husika.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuviongeza, kuviboresha na kuviendeleza vituo vya ubunifu (Innovation Hubs) kwa ajili ya kukuza ubunifu wa vijana katika mambo mbali mbali ya teknolojia.

(b) Je, ni upi mpango wa kuandaa na kutoa nafasi za kujitolea (internships) ili vijana waweze kujenga uwezo wa kikazi na kuweza kuajirika.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuziunganisha taasisi za elimu na sekta za ajira ili wanafunzi waweze kufanya mazoezi katika mazingira ya kazi wakiwa masomoni.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

157. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa muda mrefu Wizara yako imekosa Makumbusho ya Taifa.

Je, Idara ya Mambo ya Kale kwa sasa inatumia jengo gani kama ni ishara ya Makumbusho ya Taifa.

# III. HOJA ZA SERIKALI:

## Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2023/2024.

**Waziri wa Maji, Nishati na Madini:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
08 Juni, 2023. **KATIBU WA BARAZA**